JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
BARAZA ZA SANAA LA TAIFA (BASATA)

Simu: 255 22 2863748
Barua pepe: info@basata.go.tz
Tovuti: www.basata.go.tz

Ilala Sharif Shamba,
P.O. Box 4779,
Dar es Salaam, Tanzania

MWONGOZO WA KUZINGATIWA WAKATI WA KUENDESHA SHUGHULI ZA SANAA NA BURUDANI KATIKA KIPINDI CHOTE CHA MLIPUKO WA *COVID -19* NCHINI

1.0 Utangulizi

Kufuatia kuwepo kwa ugonjwa wa *CoVID-19* unaotokana na Virusi vya Corona nchini ambao ulioripotiwa kwa mara ya kwanza mwezi Machi, 2020, Serikali iliamua kusimamisha shughuli zote za Sanaa na Burudani kwa lengo la kupunguza kuenea kwa ugonjwa huo. Takwimu za mwenendo wa ugonjwa wa *CoVID-19* nchini kwa sasa zinaonesha kupungua kwa maambukizi na wagonjwa jambo ambalo linaleta matumaini ya kuendelea na shughuli za kijamii na kiuchumi, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliruhusu shughuli za Michezo kuendelea kuanzia Juni Mosi, 2020. Pia ameruhusu shughuli zingine zikiwemo shughuli za sanaa kuanzia Juni 29, 2020. Aidha, Mhe. Rais aliagiza watu wote tuendelee kuzingatia miongozo inayotolewa kuhusiana na namna ya kujikinga na Corona.

Kwa maelekezo hayo, Baraza la Sanaa la Taifa kwa kuwashirikisha wasanii na wadau mbalimbali wa Sanaa na Burudani yakiwemo mashirikisho ya sanaa, vyama, wamiliki wa baa, kumbi za sherehe na burudani, wasanii na wadau wa sanaa wamekubaliana kuzingatia kufuata mwongozo huu, baada ya kufanyika kikao cha pamoja Mei 28, 2020 katika ukumbi wa BASATA ambapo maoni yaliyotolewa na wadau hawa yalisaidia kupatikana kwa mwongozo huu.

2.0 Mambo ya Kuzingatia

Utaratibu huu unalenga kusaidia uwepo wa mazingira wezeshi na salama ili kuendelea na Shughuli za sanaa na Burudani na kuepusha kuenea kwa maambukizi ya Virusi vya Corona.

Aidha utaratibu huu utatumika ndani ya Tanzania Bara kwa Shughuli zote za sherehe, sanaa na burudani za aina zote na katika ngazi zote.

Katika kufanikisha uwepo wa mazingira hayo yafuatayo ni muhimu kuzingatiwa.

2.0.1 Elimu kwa wadau wa Sanaa na Burudani kuhusu kujikinga na maambukizi:

a) Wataalam wa afya kwa kushirikiana na maafisa utamaduni, wasimamizi wa Sanaa watoe elimu kwa wadau wa Sanaa na Burudani kuhusu kujikinga na maambukizi ya virusi vya Corona kabla Sanaa na Burudani yoyote haijaanza rasmi ikiwemo kuhusu Mwongozo huu na maelekezo mengine ya wataalamu wa afya;
b) Ushirikishwaji wa Maafisa utamaduni, Maafisa afya wa kata, watendaji wa kata, vijiji na mitaa katika kukagua na kusisitiza uzingatiaji wa masharti ya afya dhidi ya maambukizi ya corona katika kumbi za sherehe na burudani.
c) Mshereheshaji anawajibika kuwakumbusha waalikwa mara kwa mara namna ya kujikinga na maambukizi kwa kuzitaja njia sahihi zilizoelekezwa na wizara ya afya.
d) Kila baada ya tukio wasanii watoe elimu kuwakumbusha wadau kuzingatia maelekezo ya kujikinga na ugonjwa wa Corona. Aidha mabango yawekwe pia katika maeneo yote yatakayohusisha wananchi kuangalia Burudani;
e) DJs, MCs na wasanii washiriki kikamilifu kutoa elimu na kusisitizia tahadhari za kiafya kila wanapopata nafasi;
f) Matangazo na machapisho yote yazingatie pia kuwezesha makundi yenye mahitaji maalum kupata elimu husika.

2.0.2 Kumbi za Sherehe na Burudani, Maeneo ya Burudani na Mazoezi (Location)

i. Wamiliki wa kumbi za sherehe na burudani pamoja na uongozi wa viwanja vya wazi vinavyotumika kwa shughuli za burudani waweke miundio mbinu ya kuwezesha upatikanaji wa maji tiririka na sabuni kwa ajili ya kunawia mikono au vipukusi (*sanitizers*) katika maeneo yote muhimu kwa ajili ya kujikinga na maambukizi;
ii. Kuzingatia miongozo inayotolewa na wataalam wa Wizara ya afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.
    - Kupima joto la kila mdau/mteja ambaye ataenda katika maeneo ya burudani
    - Matumizi ya vitakasa mikono na maji tiririka
    - Uvaaji wa barakoa

- Kuzingatia umbali wa mita moja wakati wa ukaaji kati ya mtu mmoja na mwingine (Social distance)

iii. Milango yote ya kuingiza watu kwenye matamasha ifunguliwe mapema na itumike kwa kuzingatia umbali wa mita moja wakati wa kuingia na kutoka ili kuepusha misongamano na uwepo wa vitakasa mikono.

iv. Kupunguza idadi ya wateja/wadau katika baa na kumbi za sherehe kwa kuweka viti vichache kuliko idadi ya kawaida. (Ukumbi uwe na nusu ya jumla ya idadi ya wageni wanaotakiwa kuingia ukumbini mfano 150/300)

v. Kupunguza idadi ya wasanii wakati wa kurekodi kazi zao (wanapokuwa Location).

vi. Matumizi ya mitandao ya kijamii kuonyesha/ kufanya matamasha na kuuza kazi za sanaa.

vii. Nyakati za usiku watoto wasiruhusiwe kuwa katika kumbi za sherehe na burudani.

viii. Wakati wa utoaji zawadi uwe kwa utaratibu ambao hautaruhusu watu kugusana na kakaribiana au zawadi zote zitolewe mlangoni wakati wahusika wanaingia ukumbini.

ix. Kuwatakia maharusi maisha marefu (cheers) ifanyike kwa meza/ watu walipo kusiwe na mizunguko kama ilivyozoeleka.

x. Wakati wa kucheza muziki kwenye sherehe, MCs anyanyue meza moja baada ya nyingine ili kupunguza msongamano wakati wa kucheza.

xi. Ili kupunguza msongamano katika kumbi na maeneo ya burudani, matumizi ya maeneo ya wazi kwa ajili ya kufanya shughuli za sanaa hususan muziki zitumike ili kupunguza msongamano katika kumbi na baa.

xii. Kuwe na ukomo wa muda wa sherehe kufanyika isiwe zaidi ya saa 6 usiku.

xiii. Wenye viti na watendaji wa mitaa/vijiji waendelee kusimamia maeneo ya Sanaa na Burudani na kutoruhusu kumbi ambazo hazijasajiliwa na kupewa vibali na BASATA kutofanya shughuli zozote za sherehe na burudani.

2.0.3 Usalama wa Wasanii

i. Kwa upande wa muziki wa dansi kila msanii awe na kipaza sauti chake/ kifuniko cha kipaza sauti ili kupunguza uwezekano wa maambukizi.

ii. Wanamuziki wapewe elimu ya matumizi salama ya vyombo vya muziki (usafi).

iii. Wasanii na wadau wa sanaa watakaohisiwa/watakaojihisi kuwa na dalili za kuumwa ugonjwa wa Corona watoe taarifa ili waunganishwe na vituo vya matibabu.

iv. Wasanii watakaosafiri kwenda nje; kibali kitatolewa na Baraza kwa msanii anayekwenda nje baada ya kujiridhisha kuwa nchi anayokwenda inaruhusu wageni

kuingia na kutoka, na msanii awe na cheti cha Daktari kilichotolewa ndani ya siku kumi na nne kinachothibitisha kuwa amepimwa na hana maambukizi ya virusi vya Corona.

v. Wasanii kutoka nje, Taasisi au mtu yeyote anayemualika msanii kutoka nje anawajibu wa kuhakikisha msanii huyo na msafara wake wanatoa uthibitisho kuwa hawana maambukizi ya Corona. Na wawapo hapa nchini watalazimika kufuata na kutekeleza maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Afya kuhusu kujikinga na ugonjwa wa Corona.

2.0.4 Mazingira Mengine Wakati wa Mazoezi na Matamasha

i. Kupunguza idadi ya wasanii wanapokwenda kurekodi kazi zao (wanapokuwa Location).

ii. Mashabiki (hadhira) wanapoingia kwenye tamasha hawataruhusiwa kusababisha msongamano wakati wa kuingia uwanjani au kuwakumbatia wasanii wawapo jukwaani, aidha waandaji wa tamasha wahakikishe upo na uzio kati ya jukwaa na watazamaji kwa azma ya kuondoa ukaribu baina yao ili kuzuia kupeana mikono, kupongezana kwa kukumbatiana wakati wa tamasha;

iii. Wasanii na wadau wanapokuwa kwenye matamasha wazingatie kanuni ya mita moja kuliko kubanana kama ilivyo katika mfumo wa kawaida;

iv. Wasanii wanaposafiri kwenda kwenye matamasha mikoani wazingatie taratibu zote za kujikinga ikiwemo kuhakikisha abiria wote wamekaa kwenye viti na kunawa kwa maji tiririka au vipukusi kabla ya kuingia kwenye vyombo vya usafiri;

v. Waandaaji wa matamsha wahakikishe wasanii wawapo nyuma ya jukwaa (back stage) wanakaa umbali wa mita moja na kuweka vitakasa mikono au maji tiririka na sabuni.

2.0.5 Vifaa vya Sanaa na Burudani:

i. Vifaa vya wasanii (Magitaa, vipaza sauti, tumba, vinanda n.k) vinavyotumika wakati wa burudani vitatakiwa kusafishwa vyema kwa vipukusi (*sanitizers*) kabla na baada ya kutumika. Aidha kwa vifaa ambavyo vitaingizwa kutoka nje ya nchi kwa shughuli za Sanaa na Burudani vinalazimika kuthibitishwa usalama wake na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na Bohari ya Dawa (MSD) kabla ya kusambazwa na kuanza kutumika nchini;

ii. Kwa upande wa muziki kwa ujumla kila msanii awe na kipaza sauti chake/ kifuniko cha kipaza sauti ili kupunguza uwezekano wa maambukizi.

iii. Hatua kali zichukuliwe kwa mujibu wa Sheria za nchi na Sheria ya BASATA na kanuni zake kwa waandaaji wa shughuli za sanaa, wamiliki wa kumbi za sherehe na burudani watakaoendesha shughuli za sanaa, sherehe na burudani pasipokuwa na vibali vya BASATA na watakaokiuka mwongozo huu.

3.0 Wigo wa Matumizi ya Mwongozo:

Mwongozo huu utakoma kutumika mara tu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakapojiridhisha na kutangaza kuwa hakuna ugonjwa wa *CoVID-19* nchini.